LOWELL

PUBLIC SCHOOLS

# Kuongeza Chaguo kwa Familia

## *Mpango wa Kufungua Upya wa Shule katika Hali ya COVID-19 • Majira ya Mapukutiko 2020*







*Imeidhinishwa Agosti 5,*

# Kamati ya Shule



Safu ya Mbele: Jacqueline Doherty, Meya John J. Leahy, Andre P. Descoteau

Safu ya Nyuma: Robert Hoey, Jr., Connie A. Martin, Michael Dillon, Jr., Hilary Clark

## Imani za Kimsingi za Lowell Public Schools

- Elimu ya hali ya juu ni haki ya kimsingi ya kila mtoto tunayomhudumia.
- Kufunza na Kujifundisha ni kiini cha kazi yetu. Kila tunachofanya kinafaa kutegemeza kinachofanyika darasani.
- Wazazi ni washiriki wetu. Ni walimu wa kwanza wa wanafunzi wetu nyumbani.
- Hakuna suluhisho la kipekee la kuboresha shule zetu. Uboreshaji wa shule endelevu unahitaji kazi nyingi na thabiti kwa muda.
- Kila mtu mzima katika mfumo ni mwenye kuwajibika katika mafanikio ya wanafunzi wrtu. Kumweka kila mtoto katika mwelekeo wa kupata mafanikio katika chuo kikuu au kazi ni wajibu wa jamii nzima..

*Usawa • Ubora • Uwezeshaji*

## Ahadi za Kimsingi za Lowell Public Schools

- Toa pengo za mafanikio na fursa za kirangi, kikabila na kilugha kati ya wanafunzi wote.
- Toa kwa usawa ufadhili na rasilimali kati ya shule tofauti za wilaya.
- Shiriki na familia zote na upole, hadhi, heshima na ufahamu wa kitamaduni..

# Orodha ya Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Ujumbe kutoka Msimamizi Boyd | Kurasa 4-5 |
| Muhtasari Kuu | Ukurasa 6 |
| Kanuni za Mwongozo kwa Kuanza Mwaka wa Shule | Ukurasa 7 |
| Mafunzo kutoka Majira ya Machipuko ya 2020 | Kurasa 7-8 |
| Orodha ya Tarehe Muhimu | Ukurasa 9 |
| Kufikiria Chaguo zako za 2020-2021 | Kurasa 9-10 |
| Namna ya Kuchagua Uwekaji wako wa Shule | Kurasa 11-12 |
| Linganisho la Mafunzo ya Mbali kwa Kuhudhuria Kibinafsi | Ukurasa 13 |
| Chaguo la Mafunzo ya Mbali | Kurasa 14-15 |
| Chaguo la Kuhudhuria Shule Kibinafsi | Kurasa 16-17 |
| Nafasi ya Mwanafunzi kwa Shule | Kurasa 18-20 |
| Usafirishaji | Kurasa 21-22 |
| Vifunika Uso | Ukurasa 23 |
| Vyombo vya Kujilinda vya Kibinafsi & Vifaa za Usafishaji | Ukurasa 23 |
| Kunadhifisha & Kuua Virusi kutoka Majengo Yetu | Ukurasa 24 |
| Kalenda ya Shule Iliyoandaliwa Upya kwa Mwaka wa 2020-2021 | Kurasa 25-26 |
| Mpangilio wa Muda Nje ya Shule | Kurasa 27-28 |
| Uwezekano wa Uambukizaji wa COVID-19 Shuleni | Kurasa 29-30 |
| Rasilimali za Ziada | |
| ● Endelea Kushikamana | Ukurasa 31 |
| ● Kituo cha Rasilimali cha Familia | Ukurasa 31 |
| ● Elimu Maalum | Ukurasa 32 |
| ● Mawasiliano kwa Familia Wanaotumia Lugha Zaidi ya Mbili | Ukurasa 32 |
| ● Huduma za Lugha | Ukurasa 33 |
| ● Sheria ya McKinney-Vento | Kurasa 34-35 |
| ● Military Interstate Children's Compact Commission (Tume ya Maafikiano ya Kati ya Majimbo ya Watoto wa Jeshi) | Ukurasa 35 |
| ● Timu ya Kazi ya Kurejea Shule | Kurasa 36-47 |

# Ujumbe kutoka Msimamizi Boyd

Wapendwa Jamiii ya Lowell Public Schools:

Ninafuraha kugawa nanyi ripoti hii ambayo inatoa muhtasari wa mpango wetu wa awali wa kufungua upya mashule kwa usalama katika majira ya mapukutiko ilihali tukiboresha muundo wetu wa mafunzo ya mbali kwa familia zitakazochagua kusomea nyumbani.

Katika majira ya kiangazi, wafanyikazi wa shule ya Lowell Public Schools wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii huku wakitayarishia mwaka wa shule ujao, wakifikiria namna ya kurejelea kwa usalama kwa majengo yetu yataweza kuwa, na wakichunguza iwapo itawezekana kuwa na wanafunzi, walimu na wafanyikazi kwa darasa. Kabla ya mwisho wa mwaka wa shule uliyopita, tuliunda timu ya kazi iliyo na wakuu wa shule, walimu, wafanyikazi wasidizi na wazazi kutoka wilaya nzima kuangalia kila muundo unaowezekana wa kielimu kwa mwaka wa shule wa 2020-2021, kwa hivyo ninaamini kwamba tuko tayari kwa kila uwezekano tunayoweza kukumbana nayo kutoka Septemba na baada yake.

Mpango uliyo katika ripoti hili iliandaliwa kutoka mawazo bora zaidi ya timu ya kazi, pamoja na maoni tuliyopokea kutoka jamii – ikiwamo jawabu za utafiti kutoka zaidi ya familia 2,500 na majadiliano ya mbali na zaidi ya wazazi, wafanyikazi na wanafunzi 1,000 katika baraza za kijamii. Tunatambua kwamba ripoti hili la awali halijibu maswali zote kuhusu kufunguliwa upya wa shule. Tafadhali jua kwamba maelezo zaidi yatatolewa kabla ya siku ya kwanza ya shule.

Kwa sasa uamuzi wa namna ya kuenda mbele kwa kuanza mwaka wa shule wa 2020-2021 ni uamuzi wa kijimbo. Na hapa Lowell, ni wazi kwamba familia wanataka chaguo kuhusu namna tutarejelea shule Septemba. Tukiwa tunaelewa hili, na iwapo data ya afya ya jimbo iendelee kuenda kwa mwelekeo sawa na iwe salama kwa wanafunzi wetu kuwa shuleni, **tuko tayari kuwapatia familia zetu chaguo la masomo ya muda kamili, ya mafunzo ya mbali au mafunzo kamili ya kuwa shuleni katika mwanzo wa mwaka wa shule.**

COVID-19 bado ni sababu ya wasiwasi huku Massachusetts, lakini jimbo hili – ambalo kwa mara lilikuwa kituo cha virusi hili – sasa limo katika hali nzuri zaidi kuliko kote nchini kwa sababu tumechukuwa hatua kubwa ili kupinga kuenea kwake. Kurudi wa kikamili kwa shule unamaanisha kwamba tutaendelea kufuata miongozo madhubuti ya kiafya – kuvaa barakoa, kupeana umbali wa kijamii na kulinda usafi wa majengo yetu. Hatuwezi – na hatutaweza – kulegea panapohusu afya ya wanafunzi, wafanyikazi au jamii yetu. Hatutafuti ulegevu katika kufuata itifaki za kiusalama – tutalinda umbali wa futi sita wakati wote. Pia tutaweka kikomo katika miingiliano ya vikundi vya wanafunzi na vikundi vingine. Kwa uwezekano mkubwa hatutakuwa tukila chakula cha mchana katika mkahawa au kufanya mikutano mikubwa kwa mfano.

Ingawa data ya sasa inapendekeza kwamba tunaweza kurejelea kwa usalama kwa madarasa za majengo yetu, tunajua kwamba siyo familia zote huhisi vizuri kutuma mtoto wake sasa hivi. Kwa hivyo, zaidi ya uwezo wa kurejelea kwa shule, tutawapatia wanafunzi wetu chaguo ya mafunzo ya mbali.

Marudio ya mafunzo ya mbali yatakuwa tofauti na tuliyoona majira ya machipuko. Wilaya imenunua vifaa vya kutosha ili kila mwanafunzi apate kifaa mmoja mwaka wa shule ujao. Kutakua na jukwaa thabiti ya kiteknolojia kwa kila kiwango darasa na kuhudhuria unaohitajika, pamoja na maoni zaidi kwa wanafunzi kupitia daraja la matokeo ya kawaida zaidi.

Kukuza chaguo hizi mbili kwa familia na kufikia uamuzi kuhusu kitakachowezekana kwa wanafunzi wetu mwezi wa Septemba haikua kazi rahisi. Tunajua kwamba hakuna kinachoweza kuchukua nafasi ya miingiliano ya kila siku ya moja kwa moja ambazo walimu wetu hupata na wanafunzi. Lakini miingiliano hii ya moja kwa moja yataweza kutendeka kwa pekee iwapo tu ni salama kurejea shuleni. Tulikuwa na matumaini kuwa janga hili lingekuwa limeisha kufikia muda huu, lakini kwa bahati mbaya bado haijakuwa hivyo.

Kuwapatia familia chaguo za uwezo wa mafunzo ya moja kwa moja au mafunzo ya mbali ni uamuzi unaoungwa mkono na data ya kiafya na uamuzi uliyofanywa baada ya mchakato wa mpango ukiyofikiriwa na uliyo pana. Kwa hivyo, iwapo itakuwa kwa kufanya kiingilio kwa mbali au kwa kurejelea darasani wa moja kwa moja, tuko tayari kumpatia mtoto wako mazoea ya kimaana ya kielimu kuanzia mwaka wa shule wa 2020-2021.

Nina imani kwamba mwaka wa 2020-2021 utakuwa mwaka wa shule bora sana kwa kila mmoja wa wanafunzi wetu 14,500. Ninatarajia kuwakaribisha wanafunzi wetu kurejelea shule katika majira ya mapukutiko - hata ikiwa kwa mbali – na tuna fahari na unyenyekevu kuwahudumia kama msimamizi wenu.

Wako Mwaminifu,

Dr. Joel D. Boyd
Msimamizi wa Mashule

# Muhtasari Kuu

Mpango wa kufunguliwa upya wa Shule ya Lowell Public Schools unaupea kipaumbele usalama wa wanafunzi na wafanyikazi na umeundwa kuongeza chaguo za familia, huku ikitoa chaguo baina ya mafunzo ya mbali au mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi. Ni muhimu kusoma kwa makini ripoti hii na kufahamu namna ya kuchagua chaguo linalofaa zaidi mahitaji ya familia fulani. LPS pia itatekeleza mikutano kadhaa ya kuarifu ili kusaidia familia kufahamu chaguo zao.

Siku ya kwanza ya shule katika Lowell imepangiwa kuwa Septemba 17. Iwapo familia ingependelea mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi shuleni, wanafaa kuchagua hivyo kupitia ombi. Muda wa ombi ni Agosti 19 - Agosti 27, 2020. Familia zinazotaka kushiriki katika mafunzo ya mbali hawafai kujaza ombi.

Iwapo familia wengi zaidi watachagua kuhudhuria kibinafsi kuliko nafasi zilizopo (kwa msingi wa nafasi zilizorejelewa upya kwa sababu ya umbali wa kijamii na itifaki za usalama), bahati nasibu itafanyika ili kuamua ni nani ataweza kuhudhuria shule kibinafsi. Nafasi ya mwanafunzi katika bahati nasibu itaamuliwa na mfumo wa uzani. Familia zinazochagua mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi wataarifiwa kuhusu uwekaji wao katika mwaka wa shule wa 2020-2021 kuanzia Septemba 4.

Tunawahimiza wanafunzi kutembea au kutumia gari kufika shule badala ya kutumia basi la shule, ili kuongeza usalama na kukomesha uambukizi wa wanafunzi wengine kuenda na kutoka shule kila siku. Usafirishaji wa kutumia basi la shule utapatikana kwa wale wasio na njia nyingine ya kufika shule. Iwapo mahitaji ya usafirishaji yatakuwa zaidi ya idadi ya viti zinazoweza kupatikana, LPS itafanya bahati nasibu ya viti zinazoweza kupatikana kutumia mbinu ya uzani inayozingatia haki za kisheria za wanafunzi wanaolindwa na mazingatio ya usawa.

Uamuzi wako kwa mwaka wa shule wa 2020-2021 hauta athiri mpango wa uwekaji wa mtoto wako katika miaka shule ijayo. Mtoto wako bado atakuwa na nafasi katika shule aliyokuwa anasomea mwaka wa shule 2019-2020, au katika hali ya mwanafunzi wa shule ya msingi kuendelea mbele katika shule ya kati, bado atakuwa na nafasi katika shule ya kati aliyepangiwa kuingia.

Chaguo la mafunzo ya mbali ina jadwali iliyopangwa iliyo na masharti za kuhudhuria na kushiriki. Wanafunzi watapewa alama kupitia mizani ya kawaida. Ina mchanganyiko wa mafunzo ya moja kwa moja kwa mbali na kujifunza huru katika masomo kadhaa, pamoja na tathmini iliyo na msingi ya mradi na mtihani uliyolindwa wa mtandao. Sehemu za chakula za chukua na uende zitaweza kupatikana.

Chaguo la kuhudhuria kibinafsi lina jadwali la kawaida na mtaala uliyo na tathmini na kutoa alama ya kawaida. Kutakuwa na mabadiliko ndogo ya kimasomo ili kuzingatia usalama na umbali wa kijamii – wanafunzi na wafanyikazi ni lazima wavae barakoa; wanafunzi watakaa na kundi/darasa lao pekee; na wanafunzi watakula katika madarasa yao.

Bila kujali iwapo mwanafunzi atachagua kuhudhuria kibinafsi, au afanye mafunzo ya mbali, wilaya katika msimu huu wa kiangazi ulinunua vifaa vya kutosha ili wanafunzi wote wa LPS watapokea vifaa vyao kibinafsi mwaka wa shule huu.

## Kanuni za Mwongozo kwa Kuanza Mwaka wa Shule

1. Maamuzi yetu yataongozwa na data ya mwisho ya kiafya na maoni kutoka wataalam wa afya ya umma. Tutaendelea kufuatilia viwango vya visa vya ugonjwa hapa Lowell na kote katika jimbo.

2. Tutapanua chaguo kwa familia na tutatoa chaguo cha funzo la mbali, pamoja na chaguo la mafunzo ya darasani ili mradi data ya kiafya inaendelea kuunga mkono kukuwa darasani.

3. Tunatoa ahadi wa usawa, tukiwa na imani kwamba elimu ya umma ni haki ya kimsingi ya mwananchi. Familia na wanafunzi ambao kihistoria hawajahudumiwa wamekuwa na sauti katika mchakato wa mpango na watatimiziwa mahitaji yao.

## Mafunzo kutoka Majira ya Machipuko ya 2020

Tunapoendelea na mpango wa mwanzo wa mwaka wa shule wa 2020-2021, ni muhimu kuangalia nyuma na kuangazia kwa mafunzo tuliyopata kutoka kufungwa wa shule majira ya machipuko iliyopita. Kujifunza kutoka mazoea haya yametutayarisha zaidi kwa uwezekano wa mafunzo ya mbali kuendelea mbele.

**Muundo wa Mafunzo**

- Utekelezaji wenye uthabiti wa jadwali ya mafunzo ya kote jimbo iliyo na mafunzo ya mbali zaidi kwa wanafunzi.
- Jukwaa lenye uthabiti la kujifunza na mawasiliano kote jimbo kwa mazingira ya mafunzo ya mbali.
- Mafunzo ya ziada ya kijamii na kihisia (SEL) katika miundo yote ili kutegemeza mahitaji ya mwanafunzi.

# Mafunzo kutoka Majira ya Machipuko ya 2020

**Usawa kwa Wote**

- Kutoa teknolojia na uunganishi kwa familia wanaodhihirisha mahitaji ili wanafunzi wote waweze kushiriki kwa usawa katika mazingira ya mafunzo ya mbali.
- Fanya uhasibu wa COVID-19 na namna hili huathiri uwezo wa mwanafunzi kushiriki kwa usawa katika mafunzo ya mtandao, ikiwa na uwezekano wa kupanua vipengo vya mafanikio.

**Mawasiliano**

- Toa fursa kwa mawasiliano ya pande mbili na washika dau wote ili kutegemeza ukuzaji wa mipango na kufuatilia utekelezaji.
- Ujumbe wa mara kwa mara na wenye uthabiti kutika dara za shule kwa washikadau.
- Ukalimani wa matamshi na tafsiri zilizoandikwa zinafaa kupatikana na familia wanazozihitaji.

**Mazoea ya Kufunza**

- Patia wafanyikazi muda ili kupanga na kufanya kazi katika timu za ushiriki.
- Ukuzaji endelevu wa kitaaluma ili kuimarisha mafunzo ya mbali.
- Sera za kutoa alama, kushiriki na kuhudhuria zinafaa kuundwa kwa makini ili kuhakikisha ushiriki thabiti wa mwanafunzi.

**Teknolojia na Miundombinu**

- Ugawaji wa laptop kwa wanafunzi wote na sehemu za kupata mtadao kwa familia ili kutegemeza upataji wa masomo ya mtandao kwa mwanafunzi.
- Jukwa thabiti za mafunzo kwa wanafunzi na walimu katika kila darasa.

**Utegemezi kwa Wafanyikazi**

Ukuzaji wa kitaaluma endelevu kwa wasimamizi, walimu na wafanyikazi wasaidizi.

# Kufikiria Chaguo zako za 2020-2021

Kuwa na habari na uendelee kujishirikisha!

• Hakikisha umejisajili kwa arifu za baruapepe, fuata LPS katika mitandao ya kijamii na fuatilia tovuti ya LPS

• Hudhuria mkutano wa taarifa kuhusu Mpango wa Kujifunza wa LPS kwa mwanzo wa mwaka wa shule wa 2020-2021. Jadwali itagawaliwa na familia itakapomalizwa.

Soma hati hili lote (Mpango wa Kufungua Shule kwa Kisalama kwa wanafunzi)

Amua iwapo mafunzo ya moja kwa moja au ya mbali ndiyo bora zaidi kwa kila mmoja wa watoto wako na familia yako

Tamka iwapo unataka mafunzo ya moja kwa moja au mafunzo ya mbali katika muda wa kuchagua (Agosti 19-27)

## Tarehe Muhimu

- **Agosti 19 -** Fomu ya kushiriki kwa masomo ya kawaida yataweza kupatikana kutoka tarehe hili na kutumwa kwa familia.
- **Agosti 27 –** Tarehe ya mwisho ya familia kuwasilisha fomu ya kushiriki kwa masomo ya kawaida.
- **Septemba 4 –** Kuanzia tarehe hii, families watajulishwa kuhusu shule waliopangiliwa.
- **Septemba 17 -** Siku ya kwanza ya shule, baada ya kupata idhini kutoka jimbo.
- **Itaamuliwa –** Hudhuria mkutano wa taarifa kuhusu Mpango wa Kujifunza wa LPS

# Kufikiria Chaguo zako za 2020-2021

Mpango wa kufungiliwa upya wa Lowell Public Schools ni kuhusu kuongeza chaguo kwa familia kwa usalama. LPS itatoa chaguo la kuenda darasani kama kawaida mradi data ya kiafya itaendelea kutukubalia kuwa madarasani. Ripoti hii itawapatia familia taarifa wanaohitaji ili kuchukua uamuzi huu. Unapofikiria chaguo zako za mwanzo wa mwaka wa shule, tafadhali zingatia yafuatayo:

- Kila mwanafunzi ataweza kushiriki katika mafunzo ya mbali. Hakuna kikomo katika usajili wa mafunzo ya mbali. Lakini kwa sababu ya mwongozo thabiti wa umbali wa kijamii, nafasi ya kawaida ya shule kwa masomo ya kawaida utapunguka. Kwa hivyo, siyo kila mwanafunzi ataweza kuhudhira darasa shuleni. Iwapo wanafunzi wengi zaidi watajiandikisha kuja shule kuliko nafasi zilizoko, tutakuwa na bahati nasibu kuamua nani ataweza kuhudhuria shule. Kwa taarifa zaidi kuhusu mchakato huu, angalia ukurasa 10-11.

- Tunawahimiza wanafunzi kutembea au kutumia gari kufika shuleni pasi na kuchukua basi la shule, ili kuongeza usalama na kukomesha uambukizi wa wanafunzi wengine kwenda shule na kurudi kila siku. Usafirishaji na basi la shule utapatikana kwa wale wanafunzi pekee wasiyo na njia nyingine ya kwenda shuleni. Kwa taarifa zaidi kuhusu usafirishaji, angalia ukurasa wa 21.

- Uamuzi wako wa mwaka wa shule wa 2020-2021 hautaathiri mpango wa uwekaji wa shule wa mtoto wako miaka ya shule ijayo. Mtoto wako bado atakuwa na nafasi yake katika shule aliyekuwa akihudhuria katika 2019-2020, au katika hali ya mwanafunzi wa shule ya msingi kuendelea katika shule ya kati, nafasi katika shule aliyekuwa anafaa kuhudhuria katika shule ya kati haitabadilika.

Mazingatio mengine ambayo yanafaa kukusaidia kuchukua uamuzi bora zaidi kwa mtoto wako na familia yako:

- Mahitaji ya kibinafsi ya kusoma ya mtoto wako? Je mahitaji hayo yanaweza kukidhiwa na kuenda darasani au kwa mafunzo ya mbali?

- Je mtoto wako atakuwa na ufuatiliwaji na mtu mzima kwa siku ili kutegemeza mchakato wa mafunzo ya mbali au je mtoto wako atahitaji utunzaji wa mtoto?

- Je utahitaji usafirishaji na basi kwenda shule ili kuhudhuria shule kibinafsi? nafasi ya basi itakuwa yenye kikomo na wanafunzi hawatapatiwa uhakikishaji wa kusafirishwa. Familia wataweza kuwajibika kusafirisha watoto wao kwenda shule na kurudi kila siku. Kwa taarifa zaidi kuhusu usafirishaji, tazama kurasa 20-21.

- Je kuna wasiwasi za kiafya kwa mtoto wako au kwa watu katika familia yako ya karibu?

# Namna ya Kuchagua Uwekaji wako wa Shule

- Chaguo la kwanza kwa wanafunzi wote ni mafunzo ya mbali.

- Iwapo familia watapendelea mafunzo ya moja kwa moja shuleni, watahitaji kuchagua kuhudhuria kupitia ombi. LPS itachapisha fomu hili la ombi katika tovuti la wilaya na watasambaza fomu hili kwa baruapepe na katika mtandao wa jamii. Muda la ombi litakuwa kutoka Agosti 19 - Agosti 27, 2020. Familia zinazopendelea kushiriki katika mafunzo ya mbali hawahitajiki kujaza ombi. Ni muhimu familia zitathmini chaguo, zihudhurie mkutano wa kuarifiwa na wawasiliane na Kituo cha Rasilimali cha Familia wakiwa na maswali yeyote kabla ya kuwasilisha fomu zao, kwa sababu tunaomba fomu ziwasilishwe mara moja kwa kila mtoto anayesomea katika shule ya Lowell Public Schools.

- Iwapo familia zaidi ya nafasi zinazopatikana watachagua kuhudhuria shule (kulingana na nafasi zilizorejelewa upya), bahati nasibu itafanyika ili kuamua ni nani ataweza kuhudhuria shule kibinafsi.

- Nafasi ya mwanafunzi katika bahati nasibu itaamuliwa na mfumo wa uzani:
    - Wanafunzi walio na Mipango za Elimu ya Kibinafsi (IEPs)
    - Wanafunzi waliotambuliwa na Mpango wa 504 (kwa urahisishaji unaohusika na masomo)
    - Wanafunzi waliotambuliwa kwa huduma za McKinney Vento
    - Wanafunzi waliotambuliwa kama Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELs)
    - Wanafunzi katika darasa za kwanza za kila kiwango (K-2; darasa la 5; darasa la 5 9)
    - Familia walio na zaidi ya mtoto mmoja anayesomea shule za Lowell Public Schools
    - Wanafunzi wa wafanyikazi wa Lowell Public Schools

- Tunawahimiza wanafunzi kutembea au kutumia gari kufika shuleni pasi na kuchukua basi la shule, ili kuongeza usalama na kukomesha uambukizi wa wanafunzi wengine kwenda shule na kurudi kila siku. Katika hali nyingi familia watawajibika kuwasafirisha watoto wao kufika na kutoka shuleni. Usafirishaji na basi la shule utapatikana kwa wale wanafunzi pekee wasiyo na njia nyingine ya kwenda shuleni. Bahati nasibu itafanyika kwa viti zenye vikomo vinavyoweza kupatikana. Kwa taarifa zaidi kuhusu usafirishaji, tazama ukurasa 20-21.

- Familia zinazopendelea mafunzo ya kuhudhuria shuleni kibinafsi katika shule iliyo katika umbali wa kutembea kutoka nyumbani kwao wanaweza kufanya ombi la kuhamia shule hiyo ili izingatiwe. Kuhamia huu kutakuwa kwa mwaka wa shule huu pekee na unategemea nafasi inayoweza kupatikana katika shule hiyo. Fomu la kuhamia utaweza kupatikana katika tovuti la wilaya na utasambazwa kwa familia.

# Namna ya Kuchagua Uwekaji wako wa Shule

- Familia walioandikisha mtoto wao kwa chekechea kati ya Mei 26-Juni 30 waliongezwa katika bahati nasibu ya chekechea. Familia waliopata nafasi kupitia bahati nasibu wataweza kuhudhuria shule hiyo katika waka wa shule wa 2021-2022. Mwaka shule huu ujao (2020-2021), wanafunzi wote wa chekechea watapangiwa katika shule ya mtaa yao – ambayo inatambuliwa kama shule iliyo katika umbali wa kutembea kutoka nyumba ya mwanafunzi. Mpango huu utakuwa kwa mwaka wa shule mmoja pekee. Kunaweza kuwa na hali maalum (mfano kama Wanafunzi walio na ndugu wakubwa zaidi katika shule waliopata nafasi kupitia bahati nasibu wataweza kukaa katika shule hilo kwa mwaka shule wa 2020-21).

- Familia wanaochagua mafunzo ya kibinafsi wataaarifiwa kuhusu uwekaji wao kwa mwaka shule wa 2020-2021 kuanzia Septemba 4.

- Iwapo familia itaomba uwekaji tofauti kwa msingi wa sababu muhimu wa kiafya au kiusalama au kwa msingi wa badiliko la hali ya familia inayosababisha kuhitaji uwekaji tofauti, wanaweza kuwasilisha rufaa kwa Afisa Mkuu wa Usawa.

- Chaguo lako la awali kuhusu mahali pa kuanzia mwaka wa shule (mafunzo ya mbali au ya kuhudhuria kibinafsi) haitakuwa chaguo la mara moja kwa mwaka shule nzima. Familia watapewa fursa kufanya chaguo lingine kila miezi mitatu.

- Mabadiliko yeyote kuhusu mahali mwanafunzi atasomea katika mwaka wa shule wa 2020-2021 ni kwa mwaka shule 2020-2021 pekee. Wanafunzi waterejelea uwekaji wao wa 2019-2020, au katika hali ya mwanafunzi wa shule ya msingi kuendelea katika shule ya kati, wataendelea katika shule ya kati waliopangiliwa katika mwaka wa shule wa 2021-2022.

# Miundo Miwili ya Muda Kamili ili Kukidhi Mahitaji ya Wanafunzi

| | Ya Mbali Kikamilifu | Ya Kawaida Darasani, Kikamilifu |
|---|---|---|
| **Darasa** | • Vifaa vya moja kwa moja – kila mwanafunzi atapokea kifaa<br><br>• Panga jadwali ya shule ikiwa na mahitaji wazi ya kuhudhuria, na kushughulika. Wanafunzi watapewa alama kupitia daraja ya kawaida.<br><br>• Changanya masomo ya mbali ya moja kwa moja & kujifunza huru katika mada kadhaa tofauti<br><br>• Tathmini iliyo na kimsingi wa mradi na mtihani wa mtandao uliyolindwa | • Jadwali ya kawaida na mtaala uliyo na mabadiliko ndogo za masomo ili kuangalia umbali wa kiusalama /kijamii<br><br>•Wanafunzi wakae katika kundi/ darasa lile lile<br><br>• Tathmini ya kawaida & kutoa alama<br><br>• Vifaa vya moja kwa moja – kila mwanafunzi atapokea kifaa |
| **Shughuli** | • Shughulikia upatikanaji wa mtandao/WiFi<br><br>• Ratibu uwasilishaji au uchukuzi wa vifaa visaidizi (kama. teknolojia ya usaidizi)<br><br>• Anaweza kushiriki katika michezo au shughuli zaidi ya mtaala zinapopatikana | • Umbali wa kijamii /miingiliano tofauti<br><br>• Wanafunzi na wafanyikazi ni lazima wavae PPE (kama. barakoa)<br><br>• Usafirishaji wenye kikomo kuliko miaka iliyopita |
| **Huduma ya Chakula** | • Sehemu za kupata na kula chakula | • Wanafunzi wala vyakula darasani |

# Chaguo la Mafunzo ya Mbali



Timu la Kazi la Mafunzo ya Mbali ya LPS – imekumbwa na wakuu wa shule, walimu, wafanyikazi na wazazi kutoka wilaya nzima – wanaofanya kazi pamoja kuunda mpango uliyotengenezwa kufanya mazingira madhubuti ya mafunzo kwa wanafunzi katika sehemu za masomo tofauti.

Mpango wa mafunzo ya mbali umeundwa kuanzisha jukwaa thabiti ya mtandao inayotengeneza madaraja kati ya walimu na familia kuhusu kazi za nyumbani, na mawasiliano ili kufanya masomo na shule kuwezekana kwa mbali kikamilifu na kuweza kufanyika kwa mbali kupitia mafunzo ya moja kwa moja na kazi huru.

Hii siyo mpango wa mafunzo ya mbali uliyotumika katika kufungwa shule kwa dharura mwaka wa shule uliyopita. Hatua la kuanzisha mpango bora zaidi wa mafunzo ya mbali ni katika wilaya kuweza kumpatia kila mwanafunzi kifaa chao kibinafsi. Mazingatio pia yatafanyiwa kwa wanafunzi walio na IEP au mipango ya 504 wanaohitaji teknolojia ya usaidizi.

Zaidi ya jukwaa thabiti ya kiteknolojia kwa kila kiwango darasa, kutakuwa na kiwango cha kuhudhuria cha sharti, pamoja na maoni zaidi kwa wanafunzi kupitia uzani wa alama wa kawaida zaidi. Mpango wa mafunzo ya mbali ya LPS utafuata masomo ya kiwango cha darasa na Mifumo ya Mtaala ya Massachusetts.

Wanafunzi wanaweza kutarajia jadwali thabiti ya mafunzo, ikiwamo masaa maalum ya masomo ya moja kwa moja na ushauri na walimu. Wafanyikazi pia watapata wakati zaidi kwa kushirikiana, mazoezi, na mikutano ya wazazi inavyohitajika.

# Chaguo la Mafunzo ya Mbali



Watu wazima wanaweza kutakiwa kuhitaji wanafunzi kupanga teknolojia katika mahali panapofaa kufanya kazi ya shule na kazi na wafanyikazi wa shule ili kuhakikisha kuhudhuria kwa mwanafunzi na ushiriki, lakini kwa ujumla, muumbo huu wa mafunzo ya mbali hayatahitaji ushiriki wa mtu mzima kama ilivyokuwa katika kufungwa shule kwa dharura.

Kiasi kubwa cha kazi kinatarajiwa kuwa mchanganyiko wa mafunzo yanayosimamiwa na mwalimu na kazi huru ya mwanafunzi huku ikifuata jadwali iliyopangwa na inayoweza kutabirika ya masomo. Mafunzo ya mbali kwa mwaka wa shule wa 2020-2021 utatumia jukwaa la mtandao uliyoundwa maalum kwa mafunzo ya mbali, inayojumuisha shughuli za kujifunza zilizoundwa ndani na kazi za nyumbani zinazolingana na viwango vya mafunzo vinavyohitajika katika kiwango cha darasa na malengo ya mafunzo.

Ilihali wanafunzi wa madarasa ya PreK-4 watakaochagua programu ya mafunzo ya mbali watapangiwa programu ya mafunzo ya mbali katika shule yao, wanafunzi wa madarasa ya 5-12 watakaoshiriki katika mafunzo ya mbali watapangiliwa katika shule mpya ya mtandao iliyoundwa upya katika wilaya.  Kwa kuzingatia shule mpya ya mtandao kwa shule za upili, tutaweza kutia makini kuwapatia mazoea bora zaidi ya mtandao kwa wanafunzi wetu, huku tukitumia hatua bora zaidi na jukwaa za kiteknolojia ili kutoa mafunzo ya mbali.  Wanafunzi wote wanaoshiriki katika shule ya mbali ya 5-12 watarejelea shule waliokuwa wakihudhuria katika mwaka shule wa 2019-2020 kwa mwaka shule ufuatao.  Uwapo shughuli za zaidi ya mtaala zitapatikana, wanafunzi wataweza kushiriki katika mjengo wa shule ambao watakuwa wamepangiwa.

Huduma za Chakula za LPS zitaendelea na sehemu zake za kusambaza chakula cha chukua na uende ili kuwategemeza wanafunzi walio katika programu yetu ya mafunzo ya mbali. Pindi itakapoamuliwa, jadwali la sehemu ya chakula itasambaziwa familia kupitia tovuti la wilaya, pamoja na kupitia simu na baruapepe.

# Chaguo la Kuhudhuria Shule Kibinafsi

Timu la Kazi la Kuhudhuria Shule Kibinafsi la LPS iliunda mpango unaotoa wito wa viwango kali zaidi za afya na usalama katika nafasi zetu za shule huku tukibadilisha vitendo vyetu vya mafunzo ili kutumia teknolojia zaidi.

Wilaya ilifanya uwekezaji mkubwa katika vifaa, jukwaa za kidijitali, na vifaa vya kibinafsi ili wanafunzi wasilazimike kugawa vifaa wakiwa shuleni. Wanafunzi wote – wa mbali au wa kibinafsi – watapokea vifaa vyao vyenyewe.  Matumizi ya teknolojia yatapunguza matumizi ya vifaa vinavyotumika kwa pamoja na wanafunzi huku ikiwarahisishia wafanyikazi kusafisha na kulinda usafi wa nafasi.

LPS itafuata kuhudhuria wa sasa, tathmini, na utoaji alama, pamoja na mafunzo yote ya kiwango cha darasa na Mifumo ya Mtaala ya Massachusetts. Mafunzo ya kijamii na kihisia utasisitizwa.



Kwa sababu tutakuwa tunafuata miongozo thabiti ya afya na usalama, ni muhimu kufahamu kwamba chaguo la kuhudhuria shule kibinafsi hakitakuwa sawa na shule ya kawaida kabla ya kufungwa kwa dharura mwaka shule uliyopita.

Wanafunzi watatakiwa kuvaa barakoa kila siku kwa shule. Jadwali zitalazimisha mapumziko ya nje ya mara kwa mara ya barakoa.

Shule zitaandaa nafasi za mafunzo ili kuhesabu futi sita za umbali kati ya dawati za wanafunzi wanaoangalia upande mmoja wote. Wanafunzi bado wataweza kuingiliana

# Chaguo la Kuhudhuria Shule Kibinafsi



na kufanya kazi pamoha, lakini watatumia teknolojia ili ifanya hivyo kiusalama. Uwekezaji wetu wa teknolojia pia utatusaidia kubadili mfumo kwa hali ya mafunzo ya mbali baadaye mwaka huu iwapo data ya kiafya itahitaji.

Mpango wetu wa kuhudhuria kibinafsi unataka taratibu pana za kiusalama. Ishara na alama za sakafu zitawekwa kuwakumbusha wanafunzi kuhusu umbali wa kimwili. Tunazo mashine za kufukiza ili kufukiza dawa za kuua virusi ndani ya kila jengo, na LPS inaunda jadwali zitakazohakikisha unadhifishaji wa vyumba mara kwa mara. Pia mpango una mapendekezo ya kunadhifisha vitu vinavyoguswa zaidi, kama vitegemezi vya ngazi, vipini vya mlango, vifaa vya choo, nk.

Wanafunzi watakula chakula zote katika darasa zao, na wafanyikazi watatumia jadwali za kupanga darasa ay kundi, kupunguza mwingiliano kundi moja linalo na kundi nyingine ili kupunguza kuambukizana. Madarasa za sanaa zinazohusiana zitakuwa katika jadwali ndefu zaidi na zitafanyika madarasani kwa wanafunzi wadogo zaidi. Tutawapanga kwa makundi kimakusudi wanafunzi wa lugha ya Kiingereza na wanafunzi wa elimu maalum ili kupunguza kuambukizana.

# *Nafasi ya Mwanafunzi kwa Shule*[1]

Tutachagua kila mara kuchagua usalama kuliko kuongeza nafasi ya wanafunzi, kwa hivyo tutafuata ulinzi wa futi 6 katika majengo ya shule zetu. Zaidi ya umbali katika kila darasa, kutakuwa na miongozo madhubuti kwa sehemu za pamoja kama barabara za ukumbi, mkahawa, sehemu la mazoezi au ukumbi ili kukomesha mwingiliano kati ya kundi tofauti za wanafunzi.




Wafanyikazi wa shughuli wamefanya uchambuzi kuamua nafasi ya kila jengo katika shule yetu huku umbali wa futi 6 ukilindwa na huku darasa pamoja na mahali za kupumzika au maabara ambayo yana uwezo wa kutumika kama madarasa yakiangaziwa. Cheti lililo kwenye ukurasa ufuatao unaonyesha data ya uandikishaji wa shule mwaka wa shule uliyopita ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wanaoweza khudhuria kila jengo mwaka wa shule huu.

Kulingana na data kutoka Utafiti wa Kurejelea Shule wa Mzazi/Mlezi,  asilimia 70.8% ya familia waliashiria kwamba iwapo shule ya mtoto wao imefunguliwa, watapanga kumtuma shule. Kwa hivyo kutumia hiyo idadi kama kiwangongezi, shule yeyote inayoweza kuchukua zaidi ya asilimia 70% ya uandikishaji wa mwaka wa 2019-2020 imewekwa alama ya kijani kibichi; shule zinazoweza kuchukua kati ya asilimia 60-70% zimewekwa alama ya manjano; na shule zinazoweza kuchukua chini ya asilimia 60% zimewekwa alama nyekundu.

Iwapo mahitaji ya muundo wa kukuja darasani kama kawaida utazidi nafasi katika shule fulani, tutatekeleza mchakato wa bahati nasibu kama ilivyoelezewa kwa ukurasa 10-11.

[1] *Picha kutoka ripoti ya "Healthy Buildings" kutoka Harvard School of Public Health.*

# *Nafasi ya Mwanafunzi kwa Shule*

Kwa mfano, shule ya msingi ya Bailey Elementary School ilikuwa na wanafunzi 481 waliojisajili mwaka wa shule uliyopita. Kuna darasa 21 za kikawaida zinazoweza kuchukua wanafunzi 12 katika kila darasa huku ikifuata itifaki za umbali wa kijamii (jumla ya wanafunzi 252). Kwa ziada, kuna vyumba vitatu za mapumziko zinazoweza kuchukua wanafunzi watano (jumla ya wanafunzi 15). Kwa hivyo, nafasi ya Bailey iliyobadilika ni 267, au asilimia 56% ya uandikishaji ulivyokuwa mwaka wa 2019-2020. Orodha kamili ya idadi ya madarasa na maabara/vyumba vya mapumziko ya kila jengo linaweza kupatikana hapa.

| Shule | Uandikishaji 2019/2020 | Nafasi Kamili Iliyokadiriwa ya Mwanafunzi kwa Shule katika Umbali wa Futi 6' | Asilimia % ya Uandikishaji wa Mwaka wa Shule 19/20 Unayoweza kuwa kwa Shule katika Umbali wa Kijamii wa Futi 6' |
|---|---|---|---|
| **Masomo ya Watu Wazima** | | | |
| **Bailey** | 481 | 267 | **55.51%** |
| **Bartlett** | 486 | 352 | **72.43%** |
| **Butler** | 566 | 272 | **48.06%** |
| **Cardinal O'Connell** | 119 | 58 | **48.74%** |
| **Daley** | 690 | 370 | **53.62%** |
| **Shule ya Mchana** | 55 | 0 | **0.00%** |
| **Greenhalge** | 496 | 294 | **59.27%** |
| **Laura Lee** | 26 | 24 | **92.31%** |
| **Leblanc** | 30 | 105 | **350.00%** |
| **Malloy** | 62 | 77 | **124.19%** |
| **Lincoln** | 504 | 340 | **67.46%** |
| **LHS** | 3004 | 2158 | **71.84%** |

## *Nafasi ya Mwanafunzi kwa Shule*

| Shule | Uandikishaji 2019/2020 | Nafasi Kamili Iliyokadiriwa ya Mwanafunzi kwa Shule katika Umbali wa Futi 6' | Asilimia % ya Uandikishaji wa Mwaka wa Shule 19/20 Unayoweza kuwa kwa Shule katika Umbali wa Kijamii wa Futi 6' |
|---|---|---|---|
| **McAuliffe** | 505 | 300 | **59.41%** |
| **McAvinnue** | 488 | 375 | **76.84%** |
| **Moody** | 237 | 165 | **69.62%** |
| **Morey** | 507 | 312 | **61.54%** |
| **Murkland** | 496 | 303 | **61.09%** |
| **Pawtucketville** | 504 | 387 | **76.79%** |
| **Pyne Arts** | 519 | 414 | **79.77%** |
| **Reilly** | 494 | 297 | **60.12%** |
| **Riverside** | 46 | 56 | **121.74%** |
| **Robinson** | 665 | 977 | **149.92%** |
| **Shaughnessy** | 486 | 285 | **58.64%** |
| **STEM Academy** | 845 | 531 | **62.84%** |
| **Stoklosa** | 670 | 384 | **57.31%** |
| **Sullivan** | 682 | 377 | **55.28%** |
| **Wang** | 710 | 380 | **53.52%** |
| **Washington** | 254 | 231 | **90.94%** |
| **Jumla** | **14627** | **10091** | **68.99%** |

# *Transportation*

Usafirishaji kwa kawaida hupatikana kwa wanafunzi wa LPS kutoka madarasa ya K-8 – kadiri ya wanafunzi 7,100 wa Lowell (takriban 5,500 kutoka LPS) walitumia huduma za usafirishaji katika mwaka wa shule wa 2019-2020. Majira yajayo ya mapukutiko, tunawahimiza wanafunzi watembee ama wakuje na gari shule badala ya kutumia basi la shule, ili kuongeza usalama na kukomesha kuhatarisha wanafunzi wengine katika harakati ya kwenda na kurudi kutoka shule kila siku. Usafirishaji wa basi utapatikana kwa wale wasio na mbinu nyingine ya kufika shuleni.

Katika 2019-2020, basi 66 zilitumika katika usafirishaji wa kawaida. Basi hizi ziliweza kuchukuwa hadi wanafunzi 52 wa shule ya kati au hadi wanafunzi 77 wa shule ya msingi.

Kulingana na mwongozo wa CDC wa sasa, wanafunzi 25 pekee wataweza kutumia basi, ambayo ni kumaanisha tutahitaji takriban basi 180. Hatuna uwezo wa kupata idadi hizo zote za basi.
Picha ifuatavo inaonyesha namna hali tofauti za umbali zinakaa kwa basi:

**Wanafunzi 71**



**Wanafunzi 24**



**Wanafunzi 12**



# *Mchakato wa Kuomba Usafirishaji*

- Pindi nafasi za idadi za usafirishaji zikiamuliwa, LPS itaanza mchakato wa kupea nafasi za viti zinazopatikana kwa wanafunzi waliochagua na waliopangiwa mafunzo ya mbali na waliotaja kwamba wanahitaji usafirishaji.

- Iwapo wanafunzi wanasomea shule nje ya umbali wa kutembea uliyopangwa na sera ya shule na sheria ya jimbo, wanaweza kutumia usafirishaji uliyotolewa na familia au kuchagua kuhamia shule iliyo katika umbali wa kutembea kutoka nyumbani kwao.

- Iwapo mahitaji ya usafirishaji yatazidi nafasi zinazopatikana za idadi za viti, LPS itafanya bahati nasibu ya viti vinavyopatikana ikitumia mbinu ya uzani inayozingatia haki za wanafunzi wanaolindwa na mazingatio ya usawa. Mifano ya Mazingatio ya Uzani:
    - Wanafunzi walio na Mipango ya Elimu ya Kibinafsi (IEPs)
    - Wanafunzi waliotambuliwa na Mpango wa 504 (kwa urahisishaji unaohusiana na mafunzo)
    - Wanafunzi waliotambuliwa kwa huduma za McKinney Vento
    - Wanafunzi waliotambuliwa kama Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELs)
    - Wanafunzi katika darasa za kwanza za kila kiwango (K-2; darasa la 5; darasa la 5 9)
    - Familia walio na zaidi ya mtoto mmoja anayesomea katika Lowell Public Schools
    - Wanafunzi wa wafanyikazi wa Lowell Public Schools personnel



## *Vifunika Uso*



Barakoa au vifuniko uso ni lazima kwa wafanyikazi wote. Barakoa pia ni lazima kwa wanafunzi katika viwango darasa vyote, kutoka chekechea hadi darasa la 12.

Barakoa za wanafunzi zitatolewa na familia, ingawa barakoa zitaweza patikana na wanafunzi iwapo watakosa. Kinga cha uso pia kinaweza kutumika na wanafunzi wasiyoweza kuvaa vifunika uso kwa sababu za kiafya, za kitabia, au za kihisia.

## *Vyombo vya Kujilinda vya Kibinafsi & Vifaa za Usafishaji*




Vyombo vya kujilinda vya kibinafsi na vifaa vya usafishaji kwa kila moja ya shule zetu zitanunuliwa, zikiwamo:

- Kiowevu cha Kuua Virusi
- Kuosha Mikono
- Vijitambaa vyenye kiowevu cha kuua virusi
- Barakoa
- Gauni
- Kinga za Uso
- Glavu
- Jadwali ya Kufukiza ndani ya jengo/madarasa (kifaa cha kufukiza kimenunuliwa tayari kwa kila shule)

Hil linamaanisha itakuwa gharama kubwa kwa wilaya, lakini moja iliyo muhimu ili kuendelea na shughuli ya shule zetu kwa usalama.

# *Kunadhifisha & Kuua Virusi kutoka Majengo Yetu*

Wafanyikazi wetu wataendelea kufanya kunadhifisha wa kuua virusi wa ziadi katika majengo yetu, kama kutumia vifaa vya kufukiza vya kuua virusi (iliyo kwenye picha hili).



Cheti hili linatoa maelezo kuhusu mara ngapi sehemu zinaguswa zaidi (kama vipini vya mlango) zitasafishwa, pamoja na fanicha na vifaa vingine vinavyopatikana madarasani.

| **Marudio ya Usafishaji** | **Mifano** |
|---|---|
| Kila siku | Dawati za darasa, meza, nafasi zinazotumika pamoja |
| Mara kadhaa kwa siku | Vipini vya mlango, swichi za stima, vitegemezi vya ngazi, vipini vya beseni, sehemu za vyoo, sehemu za mkahawa, vitufe vya lifti |
| Kati ya Matumizi | Vifaa vya kucheza, michezo, gavi za sanaam vifaa vya kufunza, kibodi, simu, printa, mashine za kunakili, viti vya basi |

# Kalenda ya Shule Iliyoandaliwa Upya kwa Mwaka wa 2020-2021

